

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI NA NNE

29 JUNI, 2022



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI NA NNE – TAREHE 29 JUNI, 2022

I. DUA:

II. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**474. MHESHIMIWA STANSLAUS SHING'OMA MABULA (NYAMAGANA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaridhia uanzishwaji wa Tarafa za Igoma na Buhongwa ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma kwa Wananchi.

**475. MHESHIMIWA ESTER EDWIN MALEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani kuruhusu wanaopata mikopo ya Halmashauri kufanya shughuli zao binafsi badala ya kuwa na mradi wa pamoja.

**476. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini ahadi ya kuipa hadhi Zahanati ya Himo kuwa Kituo cha Afya na kukarabati Vituo vya Mwika na Himo itatekelezwa.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**477. MHESHIMIWA GODWIN EMMANUEL KUNAMBI (MLIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, ni lini Serikali itaanzisha mfumo bora wa kupima utendaji kazi kwa Taasisi za Umma.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **478. MHESHIMIWA DENNIS LAZARO LONDO (MIKUMI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, kuna mpango gani kuhakikisha barabara inayotumika kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Mwendokasi SGR inakuwa ya kudumu.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **479. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka ruzuku kwenye pembejeo zote za kilimo ili Wakulima waweze kununua kwa bei ndogo.

## **WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

### **480. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Wananchi wa Nyamichele, Komarera na Murwambe watalipwa fidia ya maeneo yao yaliyochukuliwa na Mgodi wa Barrick.

### **WIZARA YA MADINI:**

### **481. MHESHIMIWA ASIA ABDULKARIMU HALAMGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu ya upandishaji thamani Madini ya Vito kwa Vijana wa Manyara hasa Mji wa Mererani.

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA  
BIASHARA:

482. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL  
SICHWALE (MOMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji,  
Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ~~ina~~ mpango gani wa kuvutia  
Wawekezaji katika kilimo cha matunda ndani  
ya Bonde la Mto Momba.

DODOMA  
29 JUNI, 2022

N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE